# HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE YAMEPITISHA MPANGO WA BAJETI YA KIASI CHA SHILINGI BILIONI 10,150.7 KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAM MBALIMBALI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA

Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mlele limepitisha Mpango wa Bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni **10,150.7** kwa ajili ya kutekeleza program mbalimbali zilizopangwa kufanyika katika ngazi ya Halmashauri ikiwa ni makusanyomatumizi kutoka vyanzo mbalimbali vya,mapato,kama Mapato ya ndani,Ruzuku ya mishahara,Ruzuku ya matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo.

Akiwasilisha Mpango wa Bajeti mbele ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Afisa Mipango na ufuatiliaji wa Halmashauri Alfred Sungura ameeleza kuwa Bajeti ya Halmashauri imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya jumla na maelekezo mahususi ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22 ulioandaliwa chini ya Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 ambao utatumika katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2021/22 ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025.

Katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka fedha 2021/22, Halmashauri imezingatia Sera na Miongozo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2020/21 – 2024/25,Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 12 mwezi Novemba, 2020Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake,Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu,Malengo ya Maendeleo Endelevu naMwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo, sanjari na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia.

,Kuhusu fedha za wafadhili wanatarajia kupata fedha za mfuko wa pamoja wa afya ,fedha za ukimwi, kuendelea kuimarisha huduma ya afya kwa Shule za Msingi,Sekondari na kwenye Zahanati na Vituo vya kutolea huduma za Afya,kuendelea kupambana ugonjwa wa Maralia, fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya TASAF.

Fedha,kutoka Benki ya Duniawanatarajia kupata kiasi cha shilingi milioni 334 kwa ajili ya mradi ya uboreshaji wa huduma za afya kwenye vyoo, katika ngazi ya fedha hizi zinategemewa kutoka Benki ya dunia. Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ni kiasi cha shilingi billion 4.9.

Mkutano huo wa Baraza laMadiwani umepitia na kujadili rasimu ya Mipango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.wajumbe walipata nafasi kujadiliana na kupitia kifungu kwa kifungu na kuridhia kuipitisha makadrio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa mstakabari wa maendeleo ya Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri yaWilaya ya Mlele Soud Mbogo, akifunga Mkutano huu amewataka kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha wanashirikiana kwa pamoja kufikia malengo waliyojiwekea, wote waungane kwa pamoja kufikia malengo waliyojiwekea.

Amempongeza Katibu Tawala Wilaya kwa kuwapa maelekezo na kukumbusha utaratibu unaonatakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa sheria.

Akizungumzia Watoto wote waliohitimu elimu ya Msingi na kufaulu kisha wakachaguliwa kujiunga na Sekondari wazazi wametakiwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano na kuhakikisha watoto hao wanakwenda Shule kuendelea na masomo ya Sekondari na asiwepo mtoto wa kukaa nyumbani badala ya kuwa Shule.

Mwl, Alexius Revocatus Kagunze niMkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mleleakizungumzia kuhusu suala la Bajeti ameeleza kuwa wameweza kupandisha bajetikutoka shilingi milioni 725 sasa wanakwenda hadi kufikia milioni 800 ya mapato ya ndani hii ni kwasababu yajitihada za makusudi zilizofanyika kuanzia mwaka 2016 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ilikuwa ikitegemea makusanyo makubwa zaidi kutoka kwenye zao la tumbaku.tumbaku ilikuwa ikitoa milioni 700 pekee yake.

Lakini tumbaku sasa wakulima wameshuka kwenye uzalishaji sasa tumbaku inakujamilioni 100 tu, sasa wameongeza jitihada wamejenga standi mpya, wamebuni mapato kupitia vyanzo vya minada,wamedhibiti mianya mbalimbali ya upotevu wamapato ikiwepo mapato ya mazao ambayo yalikuwa yakipotea sana wametengeneza mageti wamehamasisha wakulima kulima mahindi mpunga, mahindi ,kwa bidii sana na mazo mengine ya kimkakati kama Korosho ufuta na ndiyo maana sasa tunategemea kukusanya milioni 800 ambapo million 700 itatoka nje ya tumbaku hivyo kama wangekuwa na tumbaku ilikuwa inazungumzia makusanyo ya bilioni mbili.

mwisho

**Habari katika Picha .**



.Mwenyekiti wa Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe,Soud Mbogo akitoa maelekezo kwa wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Madiwani na wataalamu kuhusu kwenda kusimamia na kutekeleza na kutekeleza yale yote yaliyoelekezwa kwenye kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025. katika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipindi cha miaka mitano.



.Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Leonard Kiyungi Diwani wa **Kata ya Kamsisi** akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya Mhe **Pinda** baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Mwl, Alexius Revocatus Kagunze akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya **Mhe Pinda** baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekabidhiwa Ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano.



Diwani wa Kata ya Utende Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Deusi Bundala, akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano.



Diwani wa Kata ya Ilunde Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Martin Jeremiah Mgoloka , akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano.



.Diwani wa Kata ya **Ilela** Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Wiliam Miulah Maganga , akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya Mhe Pinda baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano



DiwaniViti Maalum Kata ya **Nsenkwa** ya Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe , akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022

wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano.


ano.

.Diwani Viti Maalum Kata ya **Inyonga** ya Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Grace Kapalila , akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano



.Diwani wa Viti Maalum Kata ya **Inyonga** Halmashauri yaWilaya ya Mlele Mhe Katoto, akipokea kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kutoka kwa Mwenyekiti CCM Wilaya baada ya kumalizika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliokuwa ukipitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekapidhiwa ilani ili waweze kwenda kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipndi cha miaka mitano



Wajumbe wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mlele wakipitia kwa umakini kablasha la rasimu ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika kikao kilichofanyika ukumbi wa mikutano Shule ya Sekondari Inyonga.



Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mlele wakimsikiliza Mwenyekiti hayupo pichani akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kikao cha Baraza muda mfupi kabla ya kuanza kupitia rasimu ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2021



4.Wataalam wa Halmashauri,wageni waalikwa wakiwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mlele wakifuatilia mkutano huo wa Baraza la Madiwani wa kupitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika kikao kilichofanyika ukumbi wa mikutano Shule ya Sekondari Inyonga.



Wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Mlele wakifuatilia kwa umakini hotuba ya Mwenyekiti wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wakati wa kupitisha Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mlele Mhe,Soud Mbogo akiongoza Mkutano wa Baraza la Madiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele wakati wa kupitia Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mkutano uliofanyika Shule ya Sekondari Inyonga.

(**Picha na Kibada Ernest Msafiri-.Afisa Habari Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE YAMEPITISHA MPANGO WA BAJETI YA KIASI CHA SHILINGI BILIONI 10,150.7 KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAM MBALIMBALI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA**

Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mlele limepitisha Mpango wa Bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni **10,150.7** kwa ajili ya kutekeleza program mbalimbali zilizopangwa kufanyika katika ngazi ya Halmashauri ikiwa ni makusanyomatumizi kutoka vyanzo mbalimbali vya,mapato,kama Mapato ya ndani,Ruzuku ya mishahara,Ruzuku ya matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo.

Akiwasilisha Mpango wa Bajeti mbele ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Afisa Mipango na ufuatiliaji wa Halmashauri Alfred Sungura ameeleza kuwa Bajeti ya Halmashauri imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya jumla na maelekezo mahususi ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22 ulioandaliwa chini ya Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 ambao utatumika katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2021/22 ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025.

Katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka fedha 2021/22, Halmashauri imezingatia Sera na Miongozo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2020/21 – 2024/25,Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 12 mwezi Novemba, 2020Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake,Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu,Malengo ya Maendeleo Endelevu naMwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo, sanjari na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia.

,Kuhusu fedha za wafadhili wanatarajia kupata fedha za mfuko wa pamoja wa afya ,fedha za ukimwi, kuendelea kuimarisha huduma ya afya kwa Shule za Msingi,Sekondari na kwenye Zahanati na Vituo vya kutolea huduma za Afya,kuendelea kupambana ugonjwa wa Maralia, fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya TASAF.

Fedha,kutoka Benki ya Duniawanatarajia kupata kiasi cha shilingi milioni 334 kwa ajili ya mradi ya uboreshaji wa huduma za afya kwenye vyoo, katika ngazi ya fedha hizi zinategemewa kutoka Benki ya dunia. Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ni kiasi cha shilingi billion 4.9.

Mkutano huo wa Baraza laMadiwani umepitia na kujadili rasimu ya Mipango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.wajumbe walipata nafasi kujadiliana na kupitia kifungu kwa kifungu na kuridhia kuipitisha makadrio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa mstakabari wa maendeleo ya Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri yaWilaya ya Mlele Soud Mbogo, akifunga Mkutano huu amewataka kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha wanashirikiana kwa pamoja kufikia malengo waliyojiwekea, wote waungane kwa pamoja kufikia malengo waliyojiwekea.

Amempongeza Katibu Tawala Wilaya kwa kuwapa maelekezo na kukumbusha utaratibu unaonatakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa sheria.

Akizungumzia Watoto wote waliohitimu elimu ya Msingi na kufaulu kisha wakachaguliwa kujiunga na Sekondari wazazi wametakiwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano na kuhakikisha watoto hao wanakwenda Shule kuendelea na masomo ya Sekondari na asiwepo mtoto wa kukaa nyumbani badala ya kuwa Shule.

Mwl, Alexius Revocatus Kagunze niMkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mleleakizungumzia kuhusu suala la Bajeti ameeleza kuwa wameweza kupandisha bajetikutoka shilingi milioni 725 sasa wanakwenda hadi kufikia milioni 800 ya mapato ya ndani hii ni kwasababu yajitihada za makusudi zilizofanyika kuanzia mwaka 2016 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ilikuwa ikitegemea makusanyo makubwa zaidi kutoka kwenye zao la tumbaku.tumbaku ilikuwa ikitoa milioni 700 pekee yake.

Lakini tumbaku sasa wakulima wameshuka kwenye uzalishaji sasa tumbaku inakujamilioni 100 tu, sasa wameongeza jitihada wamejenga standi mpya, wamebuni mapato kupitia vyanzo vya minada,wamedhibiti mianya mbalimbali ya upotevu wamapato ikiwepo mapato ya mazao ambayo yalikuwa yakipotea sana wametengeneza mageti wamehamasisha wakulima kulima mahindi mpunga, mahindi ,kwa bidii sana na mazo mengine ya kimkakati kama Korosho ufuta na ndiyo maana sasa tunategemea kukusanya milioni 800 ambapo million 700 itatoka nje ya tumbaku hivyo kama wangekuwa na tumbaku ilikuwa inazungumzia makusanyo ya bilioni mbili.

mwisho